**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Tunisia**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Jumamosi, 22 Rabi' I 1445 H** | **07/10/2023 M** | **Na: 1445/13**

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

## Enyi Jeshi la Tunisia, Msikwepe Jukumu Lenu la Kuliondoa Umbile Nyakuzi la Kiyahudi Mashujaa wa Palestina Wamelitikisa Umbile hili la Adui basi Wanusuruni na Muziangamize Nguzo zake

**(Imetafsiriwa)**

Mnamo leo asubuhi, Jumamosi, 07/10/2023, siku moja baada ya kumbukumbu ya Vita vya Oktoba, mashujaa wa Ukanda wa Gaza walizindua shambulizi la ghafla na la kufuatana ardhini, baharini, na hewani, pamoja na kurusha makombora 5,000 na mabomu ndani ya dakika 20 za kwanza, katika operesheni inayoitwa kimbunga cha Al-Aqsa. Wakati wa operesheni hii, walivamia makaazi katika Ukanda wa Gaza, na kuwaamsha watu wa Palestina na Waislamu wote kwa picha ambazo zilijaza asubuhi yao furaha, ilifufua fahari nyoyoni mwao, na ikawakumbusha kilele cha imani ya Kiislamu: Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akifanye kitendo hiki cha kishujaa kuwa utangulizi wa ushindi wa kudumu na thabiti wa kuinua bendera ya Dini na kukomboa ardhi ya Palestina.

Yanayotokea leo katika ardhi iliyobarikiwa ni taswira ya mapema ya kile kinacholisubiri umbile hili lililoshindwa mikononi mwa watoto wa Waislamu wa dhati, katika siku ambayo inaweza kuwa inakaribia wakati majeshi yaliyo kituo yatakaposonga. Pia ni dhihirisho la wazi na lisilopingika la ukweli wa "jeshi hili lisiloshindika," ambalo sio tu ni dhaifu na la kioga bali pia dhaifu kijasusi na kijeshi, lisilo weza kukabiliana na makundi yenye silaha, achilia mbali jeshi lililopangiliwa. Hili limelileta hadi kwenye kiwango fedheha ya kimataifa.

Ndani ya saa moja ya shambulizi hilo, mashujaa walikuwa wakitapakaa mitaa yake, wakizunguka kambi zake, wakichoma vifaru vyake, na kuwaburuta askari wake na mabaki yao kama kondoo. Hifadhi zake, ulinzi, na kiburi, ambayo ilitumia kuringa, havikuweza kupatikana. Liliondoa hata ndege zake za kivita kwa kuogopa kulengwa, kwa njia ya udhalilifu na ya aibu kwake na wale waliolipa ulinzi kupitia makubaliano ya uhalalishaji mahusiano.

Kwa hivyo, mashujaa wa Ardhi Iliyobarikiwa walionyesha msimamo wao juu ya kadhia ya Palestina kama watu binafsi na makundi. Operesheni ya leo ni kilele cha mapambano ya muda mrefu. Watu wa Palestina hawakujisalimisha wala kushinikiza. Wanapaza wito wao mchana na usiku kwa watoto wote wa Ummah wa Kiislamu, mbele kabisa, majeshi yaliyowekwa kwenye kambi zao. Ni nani atakayekuwa na heshima ya kuitikia wito huu kutoka kwa majeshi ya Waislamu? Ni nani atafufua urithi wa Salah ad-din na kuitakasa Ardhi Iliyobarikiwa kutokana na najisi ya Mayahudi wanyakuzi?

Kuinusuru Gaza na Palestina yote huanza kwa kufungua mipaka na vizuizi vinavyogawanya Waislamu na kuzuia umoja wao, na vile vile jihad yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu chini ya bendera ya "La Illaha illa Allah." Pia inajumuisha kushusha bendera za kitaifa zilizopandikizwa na dola za kikoloni zenyewe, ambazo zilipanda mbegu ya umbile la Kiyahudi ndani ya mwili msafi wa Ummah, katika maandalizi ya Khilafah Rashida baada ya maumivu haya makali ya uzazi na kwa ajili ya Jihad ndani ya Jeshi la Ukombozi.

**Enyi Jeshi Tukufu la Tunisia, Enyi Watu wenye Nguvu na Uwezo, Enyi viongozi wenye Ikhlasi:**

Gaza anakuiteni, al-Aqsa anakuiteni, al-Quds anakuiteni, na kila shubiri ya ardhi zinakaliwa kwa mabavu zinakuiteni. Je! Mtaitika wito? Je! Mtakuwa na heshima ya kujiunga na vita, kuelekeza silaha na vifaru vyenu kwa adui mkandamizaji kwa ajili ya kumshinda? Hapa, mashujaa wa Gaza wameshawasha cheche, wakingojea kuwasha moto kwa umbile hili ovu. Je! Mtawanusuru wakati wanatafuta nusra yenu? Je! Hamjasoma maneno ya Mwenyezi Mungu (swt): [وَإِنِ اسْتَنْصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ] **"Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia"** [Surat Al-Anfal: 72]?

Harakisheni kuiokoa Al-Aqsa yenu na ukombozi wa Bayt al-Maqdes. Harakisheni kuling'oa umbile la Kiyahudi na mukomboe Masra ya Mtume wetu wa mtukufu (saw). Harakisheni kuvunja vunja kiburi cha Mayahudi na kukomesha majigambo yao, kwa kuwa nyinyi ni watu wa nguvu, uwezo, na hadhi, na jihad itaendelea hadi Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu Mtukufu asema:

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ تَنْصُرُوا اللهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ]

**"Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu."** [Muhammad:7].

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Tunisia**

**Simu: 71345949 / 21430700 Fax: 71345950**
**Tovuti ya Hizb ut Tahrir Tunisia:** www.hizb-ut-tahrir.tn
**Pepe:** info@hizb-ut-tahrir.tn
**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info